

Mkate wa Siku

SIKU
30

NENO LA SIKU

SEPT. 2022

SIKU 01 - MITHALI 16:3 (SUV)

"Mkabidhi BWANA kazi zako, Na mawazo yako yatathibitika."

SIKU 02 - ZABURI 46:1 (BHN)

"Mungu ni kimbilio letu na nguvu yetu; yeye ni msaada wetu daima wakati wa taabu."

SIKU 03 - ISAYA 61:7b (RSUV)

"...basi katika nchi yao watamiliki maradufu; furaha yao itakuwa ya milele."

SIKU 04 - WAFILIPHI 2:13 (NEN)

"kwa maana Mungu ndiye atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema."

SIKU 05 - MALAKI 3:6a (ONEN)

"Mimi Bwana sibatiliki."

SIKU 06 - UFUNUO 1:5b (SUV)

"Yeye atupendaye na kutuoshia dhambi zetu katika damu yake."

SIKU 07 - ISAYA 14:24 (BHN)

"Mwenyezi-Mungu wa majeshi ameapa: "Kama nilivyopanga, ndivyo itakavyokuwa; kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyokamilika."

SIKU 08 - ZABURI 91:1 (NEN)

"Yeye akaaye mahali pa salama pake Yeye Aliye Juu Sana, atadumu katika uvuli wake Mwenyezi."

SIKU 09 - 1 PETRO 5:6 (ONEN)

"Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake."

SIKU 10 - WAEFESO 2:10 (SUV)

"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."

SIKU 11 - ISAYA 30:15 (BHN)

"Bwana Mungu, Mtakatifu wa Israeli, asema: "Mkinirudia na kutulia mtaokolewa; kwa utulivu na kunitumainia mtapata nguvu.""

SIKU 12 - ZABURI 16:5a (NEN)

"Bwana umeniwekea fungu langu na kikombe changu."

SIKU 13 - KUTOKA 14:14 (ONEN)

"Bwana atawapigania ninyi, nanyi mnatakiwa kutulia tu."

SIKU 14 - 2 WAKORINTHO 1:20 (SUV)

"Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni Ndiyo; tena kwa hiyo katika yeye ni Amin; Mungu apate kutukuzwa kwa sisi."

SIKU 15 - ZAKARIA 2:5 (BHN)

"Mwenyezi-Mungu asema kuwa yeye mwenyewe atakuwa ukuta wa moto kuulinda mji huo pande zote, naye atakaa humo kwa utukufu wake."

SIKU 16 - ISAYA 48:17b (SRUV)

"Mimi ni BWANA, Mungu wako, nikufundishaye ili upate faida, nikuongozaye kwa njia ikupasayo kuifuata."

SIKU 17 - ZABURI 108:13 (NEN)

“Kwa msaada wa Mungu tutapata ushindi, naye atawaponda adui zetu.”

SIKU 18 - WAEBRANIA 10:19b (ONEN)

“kwa kuwa tunao ujasiri wa kupuingia Patakatifu pa Patakatifu kwa damu ya Yesu.”

SIKU 19 - EZEKIELI 34:26b (SRUV)

“nami nitaleta manyunyu kwa wakati wake; yatakuwako manyunyu ya baraka.”

SIKU 20 - MATENDO 17:28 (SUV)

“Kwa maana ndani yake yeye tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu....”

SIKU 21 - ISAYA 43:19 (BHN)

“Tazameni, mimi ninafanya kitu kipya. Kinafanyika sasa hivi, nanyi mtaweza kukiona. Nitafanya njia nyikani, na kububujisha mito jangwani.”

SIKU 22 - ZABURI 84:12 (NEN)

” Ee Bwana Mwenye Nguvu Zote, heri ni mtu yule anayekutumaini wewe.”

SIKU 23 - AYUBU 16:19 (ONEN)

“Hata sasa shahidi wangu yuko mbinguni; wakili wangu yuko juu.”

SIKU 24 - YOHANA 6:37 (SUV)

“Wote anipao Baba watakuja kwangu; wala ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe.”

SIKU 25 - 2 NYAKATI 32:7a (BHN)

“Muwe imara na hodari. Msiogope wala msifadhaike...”

SIKU 26 - ISAYA 54:13 (NEN)

“Watoto wako wote watafundishwa na Bwana, nayo amani ya watoto wako itakuwa kuu.”

SIKU 27 - ZABURI 68:19 (ONEN)

“Sifa apewe Bwana, Mungu Mwokozi wetu, ambaye siku kwa siku hutuchukulia mizigo yetu.”

SIKU 28 - WAKOLOSAI 3:16a (SUV)

“Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote.”

SIKU 29 - HESABU 14:18a (NEN)

“Bwana si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa upendo na mwenye kusamehe dhambi na uasi.”

SIKU 30 - YEREMIA 32:40a (BHN)

“Nitafanya nao agano la milele, kwamba sitaacha kamwe kuwatendea mema.”

Makala hii imechukuliwa kutoka
www.biblesociety.ca © Haki zote zimeifadhiwa.

Tunawashukuru sana kwa kuungana na sisi kueneza Neno la Mungu hapa Tanzania na duniani kote kwa ujumla.

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania

<https://shop.biblesociety-tanzania.org/>
<https://tanzanian.bible/>
<https://biblesociety-tanzania.org>



&



Canadian Bible Society

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA
WWW.BIBLESOCIETY.CA